**Somo la 5**

**Ufahamu Humtia Mtu Nuru ya Ukweli wa Biblia**

## KANUNI ZA UFAFANUZI WA BIBLIA

"… Maandiko matakatifu … yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu" – 2 Timotheo 3:15

Biblia inafikisha mawazo yetu katika akili zetu kwa njia mbalimbali. Ina maana hasa inavyosema. Ikiwa Biblia ni ufunuo wake Mungu kwa mwanadamu, inapaswa kueleweka na mwanadamu. Na ni kwa kila mtu; sio tu kwa tabaka maalum, au wanazuoni wachache. Biblia yatuzungumzia sote, moja kwa moja na binafsi. Imelengwa ifahamike na watu yakhe. Masomo maalum si muhimu. Maneno yake yanafikisha mawazo fulani, ukitumia maneno na misemo ya kawaida. Lugha halisi ndio msingi wa Biblia.

## UNABII : MAELEZO HALISI YANATABIRI MATUKIO HALISI

Hebu tulinganishe maelezo halisi ya Biblia na matukio halisi ambayo yanarejelewa. Kwa mfano, katika kumbukumbu la Torati 28:37 (Wakielekezwa Waisraeli), twasoma –

"Nawe utakuwa ushangao, na mithali na dharau, kati ya mataifa yote huko atakuongoza BWANA."

Kutimizwa halisi kwa unabii huu na Mungu kupitia kwa Musa ni jambo linaloshuhudiwa ulimwenguni mwote katika mataifa yote na watu wote. Ukweli wa mambo ndivyo ulivyo leo kama ilivyokuwa karne nyingi zilizopita, taifa la Wayahudi lilipotawanywa ulimwenguni mwote.

Hakuna yeyote, anayeweza kusaili kupuuzwa na hali ya kuzurura kwa taifa la Wayahudi, kwa wale wanaolikubali neno la Mungu na wale wasiolikubali. Twaona unabii halisi – maneno rahisi yaliyo na maana halisi kusema yanayosema – yametimizwa kihalisia. Hebu tuangalie kitu kingine rahisi, nyepesi kuelewa unabii kuwahusu hawa watu, na sasa tugeukie Ezekieli 37:21,22 –

"Tazama, (Mimi Mungu) nitawatwaa wana wa Israeli toka kati ya mataifa walikokwenda, nami nitawakusanya pande zote, na kuwaleta katika nchi yao wenyewe; nami nitawafanya kuwa taifa moja katika nchi hiyo, juu ya milima ya Israeli; na mfalme mmoja atakuwa mfalme wao wote; wala hawatakuwa tena mataifa mawili, wala hawatagawanyikana kuwa falme mbili tena, hata milele."

Hapa tuna unabii halisi kutoka kwa Neno la Mungu, juu ya wale wale watu. Kama vile neno la Mungu kupitia kwa Musa ilivyowataja watu halisi na matukio halisi ambayo yalikuja kutukia kihalisi, kwa hivyo tunapaswa kukubali habari hizi za Ezekieli katika hali hiyo hiyo ya uhalisia. Kusema kweli, sisi kwa leo tunashuhudia mwanzo wa kutimizwa kwa unabii huu katika hali halisi, Wayahudi wanaporejea Palestina kwa kuzaliwa kwa taifa la Israel katika mwaka wa 1948.

Hebu tuangalie tena unabii kutoka kwa Mika (5:2),

“Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli” (Mika 5:2)

“Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi” (Mathayo 2:1).

Hapa tena kuna unabii halisi na rahisi unaotimizwa katika hali halisi. Ulimwengu wote wa wale wajiitao “Wakristo” wanakubali jambo hili. Kanuni ya tafsiri halisi wafaa kuzingatiwa katika Neno la Mungu, na itaonekana ndivyo ulivyo.

**TAMATHALI YA USEMI**

Kusema kweli, kanuni hii rahisi na ya busara inaeleweka; haizuii matumizi ya kawaida ya tamathali za usemi – kipengele muhimu cha lugha yoyote ile.

Twatumia tamathali za usemi kila mara katika matumizi yetu ya lugha, na hueleweka pasi na kuleta utata wowote ule katika maongezi yetu; na ndivyo ilivyo kawaida katika Biblia. Matumizi haya hayatutatizi katika mawasiliano yetu ya kila siku na yafaa yawe hivyo pia tunapoyakuta katika neno la Mungu. Yalijulikana vema na kutumiwa nyakati za Biblia, na Wayunani na Warumi waliyabandika majina kadha. Aina ya Biblia iitwayo Companion Bible kwa Kiingereza, inataja tamathali 181 zinazotumika katika Biblia.

1. **SITIARI**

**Bwana huyu ni twiga; mkewe ni chui.**

Kwa mfano, tunapata Yesu Kristo akirejelewa kama Jiwe, Tawi, Mwanakondoo, Mchungaji, na Mkate wa Uzima. Tamathali hizi zinapamba na kupanua ufahamu wetu wa mambo halisi yanayojadiliwa.

Tunapozungumzia madikteta “ wakikandamiza haki ya raia wake chini ya miguu yao,” tunachanganya lugha halisia na ile ya istiari. Lakini wote wanatuelewa, na sehemu halisi haipotei. Hakuna aliye katika hatari ya kudhania kuwa “haki” ni vitu halisi vinavyoweza kupondwapondwa kwa kukanyagwa hasa kwa miguu. Na madikteta halisi na raia wao halisi wanasalia kuwa wao kwa wasikilizaji wetu. Hivyo hivyo, “roho nyeusi” haina uhusiano wa rangi.

**UFUNGUO –**

**Istiari =** kitu kuwakilisha kingine

**Tashbihi =** kitu kufananishwa na kingine

Yaweza kuonekana kama imerahisishwa mno , tena jambo la kimsingi sana. Ni muhimu, hata hivyo, kwa maana haya mambo mepesi na yanayofuata kanuni za kawaida za matumizi ya istiari,

yanapotokea katika Biblia, yametumiwa vibaya kupotosha ukweli wa kimsingi wa neno la Mungu, na iliyo halisi imekataliwa ati kwa sababu kuna chembe cha istiari.

Kuna mifano michache hapa kuonyesha matumizi ya istiari katika Maandiko, na twagundua, ikitafsiriwa kwa busara kama tufanyavyo katika vitabu vingine, maana halisi yaonekana bayana –

"Bwana amewatwaa ninyi, na kuwatoa katika tanuu ya chuma, katika Misri" (Kumbukumbu 4:20)

Nchi ya Misri haikuwa tanuru hasa , lakini hali na mateso  waliyoyapitia Waisraeli yalikuwa kama kuwa ndani ya tanuu. Tena –

"Angalia, Bwana aleta juu yao maji ya huo mto… nayo ni mfalme wa Ashuru … naye atakuja, na kupita juu ya mifereji yake yote, atafurika juu ya kingo zake zote" (Isaya 8:7)

"BWANA atakufanya (Israeli) kuwa kichwa, wala si mkia" (Kumbukumbu 28:13).

Kwa kanuni hizi za istiari, mnyama anawekwa badala ya falme, pembe ni wafalme, maji ni watu, mito ni mataifa, mwanamke kuwa serikali za ulimwengu, n.k

Picha wazi yaonyeshwa katika Danieli 7:2-7,  Mungu anapofunulia Danieli na pia sisi matukio yote ya historia kutoka siku za Yuda kwenda Babiloni kama mateka hadi wakati ambapo Mungu ataimarisha Ufalme wake duniani. –

"…Ndipo wanyama wakubwa wanne wakatoka baharini, wote wa namna mbalimbali. Wa kwanza alikuwa kama Simba… wa pili,kama dubu… mnyama mwingine kama chui… na tazama, mnyama wanne, mwenye kutisha, mwenye nguvu, mwenye uwezo mwingi" (vifungu 2-7)

Kisha Danieli aliambiwa kwa lugha halisi wanyama hawa wanawakilisha nini - "Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani…" (idadi ya watu walio maeneo ya ulimwengu unaokaliwa) Daniel 7:17,18,27.

Kwa sheria za kawaida za lugha, hapana ugumu wowote hapa katika kufikia uamuzi kile kilichozungumziwa, kile kilicho halisi, na kile cha mafumbo.

## 2. MIFANO (PARABLES) & MIFANO ISTIARI (ALLEGORIES)

Mifano imetumiwa mara nyingi katika Biblia kuonyesha maana ya funzo muhimu au mafundisho… Yesu alitumia mifano mara nyingi sana kukuza mafundisho yake kwa lengo la kufafanua zaidi ufahamu wa wale waliokuwa na "masikio ya kusikia". Alipoulizwa na wanafunzi wake wakati fulani kwa nini alinena kwa mifano, alijibu –

“Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa.” (Mathayo 13:11)

**UFUNGUO**

**Parable –** mfano – kulinganisha vitu vinavyofanana (**Simile -** tashbihi)

**Allegory –** Istiari – kuendelea kufananisha kwa kiwakilishi (**metaphor**)

**Type(‘shadow’) –**kitu mfano wa kivuli cha kitu kikuu zaidi

### 3. UAINISHAJI AU MFANO DALILI/KIVULI

### Types or Shadows

Biblia yatumia uainishaji au mifano dalili kwa wingi sana – hasa kwa namna fulani inapomwelekezea Kristo na kazi zake. Tena lugha halisi haipuuzi panapokuwepo uainishaji au kivuli cha mtu hakiwezi kuwepo pasipokuwa na mtu halisi ambaye ni mkuu kuliko hicho kivuli.

Mfano wa matumizi ya neno “Kivuli” katika Biblia inatokea katika Waebrania 10:1 –

“Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wowote kuwakamilisha wakaribiao.”

Sehemu kubwa ya kitabu cha Waebrania kimejitolea kuonyesha jinsi dhabihu na sheria za Musa zilitumika kama kivuli cha mambo yajayo ya uhalisia – kazi ya Yesu Kristo. Hii itaelezwa kwa mapana katika masomo yanayofuatia.

Tena katika kitabu cha Wakolosai 2:16-17 –

“Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato (yaani, amri au sheria za Musa). Mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo.”

Mifano hii yaonyesha jinsi ambavyo muktadha unaeleza vizuri sana maana ya vivuli hivi kwamba hatuachwi kukisikia.

Yesu pia aliweza kutumia aina hii ya kufundishia masomo halisi, na tena hakuacha watu kuhangaikia maana. Kwa mfano:

“Na kama ilivyokuwa siku ya Nuhu (kivuli), ndivyo itakavyokuwa katika siku za mwana wa Adamu (uhalisia).” Luka 17:26

### 4. TASHHISI/UHAISHAJI

**“Tashhisi” –** kiwakilishi cha kitu kama kwamba ki hai au ni mtu

**“Metomoni” –** ambapo jina au nomino yatumika badala ya nyingine,inayoisimamia kwa namna fulani

Hutumia tamathali hii ya usemi katika mazungumzo yetu ya kila siku. Kwa mfano, huzungumzia vitu kama magari, meli, nyumba, n.k kama “mrembo”. Pia, katika tashhisi ni tamathali ya usemi ambayo inatumiwa na maandiko katika kuwasilisha ujumbe, dhana na mafundisho. Mfano ufuatao utatuelekeza:

UTAJIRI umehaishwa – umepewa uhai.

“Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili…Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.” (Mathayo 6:24)

DHAMBI imepewa uhai (imewakilishwa na bwana ambaye sisi ni watumishi wake)

“Yesu akawajibu, Amin, amin, nawambia, Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi” Yohana 8:34

“Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena. ” Warumi 6:6

HEKIMA imehaishwa –

“Heri mtu Yule aonaye hekima… Yeye (“she” kwa kingereza) ana thamani kuliko majirani: wala vyote uvitamanivyo havilingani naye(her) Mithali 3:13-15

“Wisdom hath builded her house, she hath them hewn out of her seven pillars” Proverbs 9:1

Hekima umeijenga nyumba yake (kwa kiingereza “She”), a(she)mezichonga nguzo zake saba.” Mithali 9:1 (pia angalia v 2-3)

“She hath killed her beasts” – “Amechinja nyama zake”

Mifano mingine yaweza dondolewa lakini iliyo hapo juu yatosha kugonga ndipo. Matumizi haya ya uhaishaji ni ya muhimu sana kuukumbuka maana tutashughulikia mafundisho muhimu ya Biblia baadaye katika kozi hii.

5. **METONOMI**

Metonomi ni tamathali nyingine inayotumika kila siku bila hata kufikiria. Kwa mfano, huzungumzia “kuchemka kwa sufuria” wakati ambao tunamaanisha maji au chakula kinachopikwa ambacho kiko sufuriani. Hapa “sufuria” imechukua nafasi ya “maji au chakula.”

Mifano katika Biblia inayotumia tamathali hii ya usemi ni kama:

“Basi wakawapakulia hao watu ili wale. Ikawa, walipokuwa katika kula chakula, wakapiga kelele, wakasema, Mauti imo sufuriani, Ee mtu wa Mungu. Wala hawakuweza kula ” (2 Wafalme 4:40)

Hapa “mauti” imewekwa badala ya sumu katika Sufuria ambayo ndiyo sababu ya mauti. Kwa hivyo, kwa neno “mauti” twafaa tuelewe ni “Sumu”

“Ufunuo (burden) juu ya Babeli; maono aliyoyaona Isaya mwana wa Amozi” (Isaya 13:1)

“Burden” – Ufunuo imewekwa hapa ikaashiria “burden” au ufunuo utakaokuja.

“Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akiomba ya kuwa ikiwezekana, saa hiyo imwepuke ” Marko 14:35

“Sasa roho yangu imefadhaika; nami nisemeje? Baba, uniokoe katika saa hii? Lakini ni kwa ajili ya hayo nilivyoifikia saa hii.” Yohana 12:27

Hapa “saa” imewekwa kuzungumzia mateso atakayovumilia wakati “saa” itakapotimia. Kwa hivyo, kwa “saa” tunaelewa ni “mateso”. Hiyo ni metonomi na ni vema kuelewa inapotokea katika maandiko.

6. **UASHIRIAJI**

Twapata matumizi ya uashiriaji kila mahali katika maandiko; lakini tena hapana haja ya kutatizika au kufadhaika msingi,wa uimarishaji halisi tena imara wa Neno la Mungu. Uairishaji ni njia ya kupamba uwasilishaji halisi wa ujumbe wa Ukweli wa Mungu katika mawazo yetu. Kwa mfano:

Isaya 22:22 Na ufunguo wa nyumba ya Daudi nitauweka begani mwake…

“Ufunguo” unafikisha ujumbe halisi katika mawazo yetu juu ya mamlaka aliyokabidhiwa kama mwakilishi.

Wagalatia 2:9 …Yakobo, na Kefa na yohana… walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa Shirika…

“Mkono wa kuume wa shirika” unabeba maana ya umoja, makubaliano.

Mifano hii kwa ufupi inaeleza matumizi ya uashiriaji katika Biblia, na inaonyesha hakuna ugumu wowote katika kutambua na kubainisha uashiriaji na ujumbe halisi. Hebu tuchukulie Biblia kama ni halisi wakati sheria za kawaida za lugha zaonyesha wazi kuwa ni halisi. Hatuwezi, kama wengi wafanyavyo , kukataa uhalisia wa maelezo yasiyoambatana na mawazo yao ya jadi.

Tamathali za usemi kama tulivyoangalia zinatumika ili kupanua na kuonyesha msingi halisi. Kama vile alfabeti lazima ijulikane na kufahamika kabla ya kusoma maneno, pia msingi halisi wa Maandiko utafahamika mwanzo kabla ya kuyashika na sitiari na uashiriaji, n.k

**KANUNI RAHISI YA ZIADA**

1. **Usipuuze MUKTADHA!**

Jambo la kimsingi katika kutafiti Biblia na kuitafsiri ni ile ya kuchunguza muktadha. Matatizo mengi yanayohusiana na kuelewa Biblia yanaweza kutatuliwa kwa kusoma tu vifungu kabla na /au baada ya fungu husika. Hakikisha kuwa msimamo usiotatirika katika utafsiri wa kifungu hicho. Kwa mfano, ikiwa tafsiri ya ishara inaingiana vema katika kifungu kimoja na sio katika kingine mahali ambapo muktadha ni ule ule, kuna uwezekano wa kutokea kosa katika tafsiri na maelezo ya ishara.

2. **Acha Biblia Ijitafsiri**

Jizoeshe kuangalia vifungu vinavyofanana, ukikumbuka ya kuwa Biblia haiwezi kujipinga. Kila mara angalia na kipindi cha wakati gani. Vifungu vingi vitatoa ufunguo utakaofungua milango ya kuvifahamu. Biblia ni kitabu cha mantiki; wakati kila kitu kinaingia na kueleweka, utakuwa wafuatilia vema! Kumbuka kanuni hii maana itarejelewa na kuonyeshwa mara kwa mara katika masomo yatakayofuatia. Itumie vema katika kujisomea maandiko.

3. **Tumia Biblia NZIMA**

Ili kuelewa mpango wa wokovu wa Mungu ni vema kuisoma Biblia nzima kutoka mwanzo hadi mwisho. Agano La Kale na Jipya haziachani, pana maelewano mwafaka. Yote ni ufunuo wa Mungu kwa mafundisho yetu ya lazima. Yote yamehifadhiwa na Mungu kama riziki yetu kwa wakati wetu ili tupate ujumbe unaotutia akili ya ufahamu, ili tumche na kumtii Mungu.

Kuna wale ambao wametilia shaka haja na umuhimu wa Agano la Kale, kosa baya sana laweza kutokea. Agano La Kale ndio moyo na maelezo ya Agano Jipya. Haviachani kamwe. Tukiondoa ya Kale, tunaangamiza Jipya kabisa. Yasimama na kuanguka pamoja. Hatuwezi kuelewa Jipya bila ya Kale. Paulo alimwandikia Timotheo (2 Timotheo 3:15) –

“MAANDIKO MATAKATIFU… yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu.”

Paulo alipoandika haya , MAANDIKO aliyokuwa akirejelea ni Agano la Kale!

Agano Jipya ilikuwa haijaandikwa wakati huo. Kipindi chote cha Agano Jipya, umuhimu wa Agano La Kale, na kufahamu kwake, kunatiliwa mkazo sana, kama inavyoonekana hapa:-

“(Mimi Paulo) nimesimama hata leo, hivi nikiwashuhudia wadogo na wakubwa, wala sisemi neno ila yale ambayo manabii na Musa waliyosema, kwamba yatakuwa; ya kwamba Kristo hana

budi kuteswa na ya kwamba yeye kwanza kwa kufufuliwa katika wafu atatangaza habari za nuru kwa watu wake na kwa watu wa mataifa"  (Matendo 26:22-23).

"…Ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu, nikiyaamini yote yanayopatana na torati na yaliyoandikwa katika vyuo vya manabii" (Matendo 24:14).

"Na Paulo… akahojiana nao kwa maneno ya (Agano la Kale) maandiko"  (Matendo 17:2)

"Mpate kuyakumbuka yale maneno yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu" (2 Petro 3:2)

"Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi; ambalo mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza… Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kutafsiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Takatifu " (2 Petro 1:19-21).

Yesu mwenyewe alitia mkazo kanuni hii (Yohana 5:46-47) –

"Kwa maana kama mngalimwamini Musa, mngeniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu"

Kuhusu Agano La Kale alisema:

Msingi ambao Paulo, Petro na Yesu wameuweka wafaa uwe mbinu yetu ya kuangalia Neno La Mungu – matumizi na utafiti wa Biblia nzima. Njia hii ndio msingi wa masomo yatakayofuatia Mungu akipenda.

**Maswali kwa somo la 5**

1. Fafanua maana ya "unabii."
2. Taja mfano mmoja wa unabii ambao ulitimizwa halisi.
3. Je, matumizi ya tamathali za usemi katika Biblia haiendani na kanuni za lugha halisi kama msingi wa mawasiliano?
4. Ufafanuzi wa "Sitiari" ni nini?
5. Waweza kufikiria mfano katika Biblia ambapo Sitiari imetumika?
6. Nini fafanuzi ya "mfano" (parable)?
7. Kwa nini Yesu alitumia mifano katika mafundisho yake?
8. Eleza ufafanuzii wa uanishaji/ kivuli?
9. Ni kitabu kipi katika Biblia ambacho kimetenga sehemu kubwa ya nakala yake katika kutumia uanishaji au kivuli kwa nia ya kueleza kazi ya Kristo?
10. Nini fafanuzi ya "tashhisi"
11. Taja mifano 3 ya tashhisi katika Biblia.
12. Waweza kufafanua metonomi?
13. Toa mifano ya metonomi katika Biblia.

14. Eleza uashiriaji kama inavyotumika katika Biblia
15. Ni kanuni ipi bora ya tafsiri katika utafiti wa Biblia?
16. Kwa nini?
17. Nini maana ya “Acha Biblia ijitafsiri?”
18. Kuna umuhimu katika kutumia Agano La Kale na Jipya?
19. Mitume walitumia sehemu gani ya Biblia kama msingi wa mafundisho yao?